

**Kumb.Na.MSS/J.2/VOL.I/35**

Email;marambasecondary20@gmail.com.

Mobile. 0713-337896

Jina la mwanafunzi .....

**YAH; KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021**

1.0 Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Maramba. Shule ipo umbali wa kms 50 toka Tanga Mjini na kms 3 toka Maramba mjini unatakiwa kuripoti tarehe 7/01/2021 siku ya Alhamisi saa tatu asubuhi ukiwa na mzazi/mlezi wako.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

- 2.1 Sare ya shule hii ni rangi ya kijivu kilichoiva kwa kitambaa cha suruali (wavulana) na sketi ya kijivu kilichoiva iwe ya heshima zifikie kwenye vifundo vya miguu (wasichana)
- 2.2 Kwa wasichana sketi mshono ni wa rinda box inchi kumi mbele na nyuma marinda madogo mawili mbele na nyuma baada ya rinda box (mafundi wanaelewa) belt la sketi inchi tatu.
- 2.3 Hijabu ifanane na sare za shule yaani sketi iwe ya kijivu na nusu kanzu na juba ziwe nyeupe.
- 2.4 Kila mwanafunzi awe na viatu vya **ngozi** vyeusi visivyo na kisigino, pia vya kufunga na kamba na soksi nyeupe kwa wasichana , soksi nyeusi kwa wavulana.
- 2.5 Wavulana suruali iwe ya heshima upana nchi 15 marinda 2, kila upande **atakae, shona "modo" atarudishwa siku hiyo hiyo.**
- 2.6 Mashati meupe ya mikono mifupi ya heshima kwa wavulana na kwa wasichana wasiovaa hijabu.

**3.0 MWANAFUNZI AJE NA;**

- a) Madaftari kumi (counter book ni nzuri zaidi)
- b) Kalamu ya bluu, penseli, mkebe, kifutio.

**4.0 VIFAA VYA USAFI**

- 4.1 Wavulana walete jembe na mpini wake, fyekeo (slasher) na fagio la chelewa.
  - 4.2 Wasichana walete jembe na mpini wake, fyekeo (slasher) ndoo ndogo na fagio la chelewa
- NB; Vifaa hivi ni muhimu sana**

**5.0 KANUNI NA SHERIA ZA SHULE**

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa/kusimamishwa shule.

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kudharau bendera ya taifa
- g) Kuwa mjamzito/kumpa mimba
- h) Kuo au kuolewa
- i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu wote
- j) Kukataa adhabu kwa makusudi
- k) Kuwa na simu ya mkononi
- l) Utoro

Ufafanuzi zaidi utatolewa siku ya kuripoti na mzazi/mlezi

Fomu za kiapo cha mzazi/mlezi na fomu ya hospitali zirudishwe siku ya kikao cha tar; 7/1/2021

**KARIBU SANA MARAMBA SEKONDARI**

**T. SHESHANGALI**  
**MKUU WA SHULE**

# SHULE YA SEKONDARI MARAMBA

## KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Nakiri kusoma na kuelewa sheria zote na taratibu zote zilizotolewa na shule hii

Naahidi kumsaidia mwanangu katika kumlea na kumhimiza kutii na kufuata sheria na taratibu zote za shule.

**JINA LA MZAZI/MLEZI .....**

**SAINI.....**

**NAMBA YA SIMU .....**

## KIAPO CHA MWANAFUNZI

Nakiri kusoma na kuelewa sheria zote na kanuni zote za shule nakiri kufuata na kutii sheria hizo

Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

**JINA LA MWANAFUNZI ..... SAINI**

.....

**NB;**

- I) FOMU HII ISANIWE NA MZAZI NA MWANAFUNZI NA IRUDISHWE SIKU YA KURIPOTI SHULENI
- II) FOMU YA KUPIMA AFYA (medical examination form) IMEAMBATANISHWA NYUMA YA FOMU HII, HAKIKISHA INAJAZWA NA DAKTARI WA HOSPITALI YA SERIKALI NA KURUDISHWA SHULE SIKU YA KURIPOTI.

ASANTE

**T.SHESHANGALI  
MKUU WA SHULE  
0713-337896**